BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 20 Juni, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa. Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

283. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ilichukua juhudi kubwa ya kuliboresha soko la Darajani ili liwe na hadhi ya kisasa na liwavutie watalii ambao wengi wao hufika sokoni hapo kujifunza tamaduni za Wazanzibari kupitia soko hili. Pamoja na juhudi za ujenzi wa soko hili, uchafu katika soko hili kwa sasa unatoa taswira mbaya kwa jamii pamoja na wageni, jambo ambalo linaweza kuwafanya wageni wengi kutolitembelea eneo hili.

(a) Je, vipi Serikali yetu inalifahamu tatizo la uwepo wa uchafu katika soko la Darajani.

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani ya kuweka mazingira ya usafi katika soko hili ambalo ni kioo kwa wageni wote wanaoitembelea Zanzibar.

(c) Je, ni mapato ya kiasi gani kwa mwaka hupatikana kupitia wafanyabiashara waliopo katika soko hili la Darajani.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

136. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Pamoja na ripoti za miaka ya karibuni za Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kuonyesha ukuwaji katika sekta ya fedha na faida kubwa kwa benki zinazotoa huduma zake nchini, ripoti nyingi za kitaalamu zimehusisha faida kubwa kwa benki na riba kubwa kwa mikopo wanazowatoza wateja.

(a) Je, kuna ukomo wa riba ambao BOT wameuweka kisheria kwa benki kuwatoza wateja wao kwa mikopo midogo midogo na mikopo ya kibiashara.

(b) Je, ni kwa namna gani sera ya fedha ya nchi inamjali mwananchi wa kipato cha chini katika kupata mkopo wenye riba nafuu.

(c) Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa riba kubwa zinazotozwa na taasisi za fedha (Microfinance) ambazo ndio kimbilio la wananchi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

205. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ni kwa namna gani Wizara yako inajikita vyema katika uwekezaji mzuri wa miundombinu ya uhifadhi wa chakula.

206. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tathmini iko vipi kwa sasa juu ya uzalishaji wa mazao ya biashara na upatikanaji wa fursa ya masoko kutokana na bidhaa wanazozalisha wakulima wetu.

**Wizara ya Afya:**

15. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na hospitali ya Chukwani kutoa huduma za afya kwa muda wa masaa ishirini na nne (24), hali ya hospitali hiyo hairidhishi ingawa Serikali kupitia Wizara ya Afya iliwahi kuifanyia ukarabati mkubwa kwa lengo la kuboresha huduma ya afya kwa wananchi, ukarabati ambao bado haujakamilika huku hospitali hiyo ikiendelea kukabiliwa na uhaba wa baadhi ya vitendea kazi na ukosefu wa dawa.

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kumaliza changamoto hiyo katika hospitali ya Chukwani.

55. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa madaktari hawaruhusiwi kutibu bila ya leseni na kwa kuwa kuna taarifa kwamba Daktari kutoka Zanzibar hawezi kutibu nje ya nchi mpaka apate leseni ya nchi husika.

(a) Je, ni upi utaratibu unaotumika kwa madaktari wa nje wanaokuja kufanya matibabu Zanzibar, wakiwemo madaktari wa kambi.

(b) Kwa kuwa Zanzibar kuna Baraza la Madaktari na wanatoa leseni, je, Baraza hilo linawasimamia vipi madaktari wa nje kabla ya kuwatibu Wazanzibari.

(c) Je, Baraza la Madaktari limejipanga vipi kuanzisha mfumo wa kuwasajili madaktari wao utakaosaidia kurahisisha ufuatiliaji na utendaji.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

84. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Umeshapita muda mrefu tokea ilipoahidiwa kujengwa barabara ya Mkoani – Chake Chake ambayo kwa bahati mbaya mpaka sasa bado haijajengwa wala hakuna dalili yoyote ya ujenzi wake, pamoja na kuwepo kwa taarifa kuwa mikataba ya ujenzi wake ilishafungwa.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu vipi suala hili.

(b) Ni lini wananchi wetu wategemee kuanza ujenzi wa barabara hiyo.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

39. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Je, ni lini Serikali itatoa muongozo juu ya mikakati ya udhibiti wa watoto walio chini ya umri wa miaka 18 kwa kuwalinda na vitendo vya ukatili na udhalilishaji.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

194. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

(a) Je, hali halisi ya kupatikana maji safi na salama kupitia vyanzo vyetu vya asili vya maji iko vipi kwa sasa.

(b) Uwiano ukoje baina ya mabadiliko ya tabia nchi katika vyanzo vyetu vya asili vya maji.

(c) Ni maeneo gani yameathirika zaidi kutokana na kukauka kwa vyanzo vya asili vya maji hapa Zanzibar.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

276. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Zao la karafuu bado linaonekana kuwa na umuhimu katika kuchangia uchumi wa Zanzibar. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikilalamikia bei ndogo kwenye soko la dunia.

(a) Je, ni upi wastani wa bei ya karafuu kwa tani moja kwa mwaka 2023/2024 katika soko la dunia.

(b) Je, ni kwa vigezo vipi Serikali hupendelea kuuza tani moja ya karafuu kwa Dola 7,500 badala ya Dola 9,000.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuishirikisha sekta binafsi katika kuliongezea thamani zao la karafuu.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

227. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Sekta ya Utalii ina jukumu kubwa katika kukuza uchumi na hatimae kufikia lengo la kupunguza umasikini kwa wananchi wetu.

Je ni ipi mikakati ya Wizara yako katika kubuni namna ya kuvuna masoko mapya ya utalii badala ya kuendelea kuzitegemea nchi zile zile tulizozizowea.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2024/2025.



**Zanzibar,**
**20 Juni, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**